**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**

**BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA**
**Tovuti: www.hlpc.go.tz**
**Simu: 0734005777 Barua Pepe:hlpc@afya.go.tz**

# TAARIFA KWA UMMA

## USHIRIKI WA BARAZA KWENYE KONGAMANO LA 37 LA WATAALAM WA MAABARA DODOMA

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara inapenda kuwataarifu Wataalam wote wa Maabara nchini kuwa Baraza litashiriki katika Kongamano la kisayansi la Wataalam wa Maabara litakolofanyika Jijini Dodoma katika ukumbi wa Jakaya Kikwete kuanzia tarehe 01.10.2024 hadi 04.10.2024. Kongamano hili linaratibiwa na kusimamiwa na Chama cha Wanasayansi wa Maabara za Afya (MeLSAT).

Shughuli zote za Baraza zitahamia kwa muda katika viwanja vya Jakaya Kikwete kwa siku zote. Hivyo, Msajili anawaalika Wataalam wote kutembelea Banda la Baraza la Wataalam wa Maabara kuanzia tarehe ya kuanza kongamano hadi mwisho ili kujifunza na kujua shughuli mbalimbali zinazotolewa na Baraza. Aidha, Baraza litatoa huduma na elimu kwa wataalam kuhusiana na masuala mbalimbali kama vile mafunzo endelevu, uhuishaji wa usajili na mfumo wa usajili (HPRS).

Wataalam wa Maabara mnaalikwa kushiriki kwa wingi katika kongamano hili muhimu ambapo wataalam watakaoshiriki watapata alama kumi (10) za mafunzo endelevu (CPD 10 Points).

Ofisi ya Msajili inawatakia ushiriki mwema

Imetolewa na:
Ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara
24.09.2024

HEALTH LABORATORY PRACTITIONERS COUNCIL
24 SEP 2024
P.O.Box 743
DODOMA